UCHAMBUZI WA BAJETI YA SEKTA YA KILIMO, NA UWIANO KATIKA MATUMIZI YA FEDHA ZA MFUKO WA MAENDELEO KWA WANAWAKE NA VIJANA: HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI, TANZANIA

Ripoti ya Utafiti kwa Muhtasari

1. UTANGULIZI

Idadi ya watu nchini Tanzania inaongeza kwa kasi, wengi wao wakiwa vijana. Mnamo 2018, Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni 52.5. Kwa mujibu wa ongezeko la 3.1% kila mwaka, idadi ya Watanzania inatarajiwa kufikia milioni 89.2 ifikapo mwaka 2035 (NBS, 2018). Ongezeko hili kubwa ni tishio kwa uhakika wa chakula na lishe, hivyo kuna haja ya kuongeza uzalishaji wa mazao kwa njia ya Kilimo Shadidi Endelevu (KISE). Mwongozo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango unazitaka Mamlaka ya Serikali za Mitaa Tanzania Bara kuelekeza 20% ya mapato ya ndani yatokanayo na shughuli za kilimo kutumika katika kuendeleza sekta ya kilimo. Vivyo hivyo 15% iende sekta ya mifugo na 5% kuendeleza sekta ya uvuvi. Kadhalika, kila Halmashauri imeagizwa itenge 10% kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya wanawake (4%), vijana (4%) na watu wenye ulemavu (2%). Maagizo haya yako sanjari na Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025, Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Uhakika wa Chakula Tanzania (TAFSIP) na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya II (2016/17-2020/21). Programu ya Utekelezaji wa Kilimo Shadidi Endelevu na Kujifunza Barani Afrika (SAIRLA) unaofadhiliwa na Uingereza iliwezesha uchambuzi wa bajeti ya kilimo ngazi ya Halmashauri ili kubaini kiwango cha uwekezaji wa rasilimali za umma kuendeleza sekta ya kilimo na kuinua hali ya maisha ya wanawake na vijana. Uchambuzi huo ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali (HWM), Mbeya kwa miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18. Lengo likiwa ni kuwataarifu watendaji wa Halmashauri, madiwani na wadau mbali mbali kuhusu vipaumbele katika bajeti na matumizi ya fedha za Halmashauri katika kuendeleza sekta ya kilimo, mafanikio na changamoto za utekelezaji wa bajeti, na kuchangia mawazo yanayoweza kuboresha sera na mfumo wa ugawaji wa rasilimali za umma wenye kuzingatia uwiano wa kijinsia.

2. MBINU YA UTAFITI

Takwimu zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbali mbali za kitafiti ikiwemo mahojiano na viongozi wa Halmashauri, madiwani, vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wilayani. Mapitio, uhakiki na uchambuzi wa kina wa taarifa na ripoti za fedha za Halmashauri, Mipango na Mfumo wa Matumizi kwa kipindi cha muda wa kati, yaani miaka mitatu (MTEF) ulifanywa kwa miaka mitano ya fedha mfululizo kutoka 2013/14 hadi 2018/2018.

3. MATOKEO MUHIMU

3.1 Kiasi cha fedha zilizotengwa kwa sekta ya kilimo

Katika mwaka 2013/14 jumla ya TSH 804 milioni zilielekezwa sekta ya kilimo ambayo ni 2.9% ya bajeti yote ya Halmashauri, lakini kiasi hicho kilishuka hadi kufikia 1.3% mwaka 2014/15. Miaka miwili baadaye, 2015/16 kulikuwa na ongezeko katika bajeti ya kilimo hadi kufikia 7.1% na 10.1% mwaka 2016/17. Hata hivyo bajeti hiyo ilishuka mpaka 2.9% mwaka uliofuata. Kuwepo kwa bajeti finyu na isiyotabirika ni moja kati ya sababu zinazopelekea kushindikana kuanzishwa na kumalizika kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ya kilimo kama vile uzalishaji wa mazao ya mbogamboga ambayo huleta faida kubwa ya kiuchumi na kijamii na hasa kwa wakulima wadogo (Angalia Jedwali 1).

Jedwali 1: Mwenendo wa bajeti ya kilimo katika HWM 2013/14 -2018/2019

Mwaka wa fedha	Jumla ya bajeti ya Halmashauri TSH mamillioni	Jumla ya mgawo wa kilimo TSH mamillioni	% ya ongezeko la bajeti ya kilimo	% ya bajeti ya kilimo kwa bajeti ya wilaya	% badiliko katika mgawo
2013/14	27,599.3	804.0		2.9	
2014/15	40,729.6	519.4	-35.4	1.3	-1.6
2015/16	49,123.9	3,503.3	574.5	7.1	5.8
2016/17	21,075.9	2,130.0	-39.3	10.1	3.0
2017/18	21,075.9	520.1	-75.6	2.9	-7.2

Chanzo: Idara ya mipango HWM, Desemba 2018

3.2 Vyanzo vikuu vya Mapato kwa ajili ya Bajeti ya kilimo katika HWM

HWM inapokea mapato yake kupitia vyanzo vikuu vinne ikiwemo (i) serikali kuu (CG), (ii) mchango wa Wahisani wa Maendeleo (DPs), (iii) mikopo, na (iv) vyanzo vya ndani ya Halmashauri. Jumla ya bajeti ya TSH 14.5 bilioni zilizoelekezwa ndani ya miaka mitano ili kuendeleza kilimo, sehemu kubwa ikitoka kwa mradi wa Matokeo Makubwa Sasa (47.9%) ikifuatiwa na DIDF (27.1%), DADG (19.5%) na mapato ya ndani ya Halmashauri (4.5%). Vyanzo vingine vilichangia chini ya asilimia moja ya bajeti yote. Hii ina maana kwamba sekta ya kilimo imekuwa ikitegemea kwa kiasi kikubwa gawio kutoka serikali kuu ambayo imekuwa haitabiriki hasa katika miaka ya hivi karibuni. Imeelezwa kuwa gawio kutoka kwa serikali kuu mara nyingi hutolewa kipindi cha robo ya tatu na ya nne ya mwaka wa fedha, kitendo kinachochelewesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa miezi mitatu au sita ya mwanzo wa mwaka wa fedha.

Mchanganuo wa kulinganisha sekta tano umeonesha kilimo kuwa na nafasi ya nne katika mgawo wa bajeti ya kawaida ya mwaka wa fedha 2013/14 mpaka 2017/18. Sekta ya maji iliongoza kwa gawio kubwa la bajeti (61.7%), ikifuatiwa na sekta ya afya (10.8%) na barabara vijijini (10.4%) (Angalia Mchoro 1).

Mchoro 1: Matumizi kwa kila sekta ya HWM, 2013/14-2017/18



Chanzo: Idara ya mipango, HWM, Desemba 2018

3.3 Vipaumbele katika matumizi ya fedha sekta ya kilimo

HWM imekuwa ikipokea michango kutoka vyanzo mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa Kuendeleza Kilimo Wilayani (DADP) ikiwemo Mfuko wa Wilaya wa Kuendeleza Umwagiliaji (DIDF) na Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo Wilaya (DLDF). Matokeo yameonesha kuwa asilimia kubwa ya fedha za kilimo zimekuwa zikitumika kujenga na kuendeleza miradi ya umwagiliaji. Kipaumbele cha pili ni ujenzi na kukarabati wa masoko; Vituo vya Mafunzo ya Kilimo Kata (WARC), mifugo na nyenzo nyingine (6.7%) wakati upangaji, usimamizi, ufuatiliaji na uelekezaji (2.0%) huchukua nafasi ya tatu. Makundi mengine yalipokea 1% tu au chini ya hapo (Angalia Mchoro 2). Kwa upande mwingine, takwimu zinaonesha kuwa agizo la serikali la kurudisha 20% ya mapato ya Halmashauri kwenda katika kilimo, 15% kwenda mifugo na 5% kwa ajili ya sekta ya uvuvi halikuwahi kutekelezwa ipasavyo wilayani Mbarali.

Mchoro 2: Matumizi kwa kutoa kipaumbele katika kilimo HWM, 2013/14-2017/18



Chanzo: Ofisi ya Afisa Kilimo, HWM, Desemba 2018

3.4 Mgawo na matumizi ya 10% ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana

Wakazi wengi wa Wilaya ya Mbarali ni wanawake (51.5%) na vijana (32%). Hivyo basi, kuwezesha upatikanaji rahisi wa fedha na mitaji kwa wanawake na vijana ni muhimu katika maendeleo ya uzalishaji wa mazao kwa lengo la kupunguza umasikini na njaa. Kwa miaka mitano iliyopita, serikali imekuwa ikisisitiza kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa itenge 10% ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuwezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata mitaji ya kuendesha miradi yao ya maendeleo katika maeneo yao. Aidha, miongozo ya serikali inaelekeza Halmashauri hizi kugawa 4% za mapato hayo kwa wanawake, 4% kwa vijana na 2% iliyobaki kwa watu wenye ulemavu. Hivi karibuni serikali imeanzisha ukaguzi maalumu wa mahesabu haya ya mgawo wa 10% ambapo

Halmashauri zisizotekeleza maelekezo hayo huhesabiwa kuwa wametenda "kosa la jinai."

Kati ya mwaka 2013/14 na 2017/18, HWM ilitoa TSH 526.8 milioni kwa MMWV ambayo ni sawa na 4.5% ya jumla ya fedha zote zilizokusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri. Kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2015/16 hakukuwa na mgawo wowote wa bajeti kwenda MMWV, lakini katika mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri ilitoa 9.5% ya jumla ya vyanzo vyake kwa wanawake na vijana. Vivyo hivyo mwaka 2017/18 Halmashauri iliweka 9.5% ya mapato yake kwenye MMWV. Kwa miaka miwili iliyopita, mgawo wa HWM kwenda MMWV umekuwa chini kidogo ya 10% inayotakiwa (Angalia Jedwali 3). Hii inaonesha kuwa miongozo ya serikali kuhusu kutenga 10% ya mapato ya ndani kwa ajili ya MMWV haukutelezwa ipasavyo.

Jedwali 3:Mgawo wa fedha za MMWV kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

Mwaka wa fedha	Jumla ya Vyanzo Halisi	Gawio kwa Vijana toka mapato ya ndani	Gawio kwa Wanawake toka mapato ya ndani	Gawio kwa Walemavu	Jumla ya mgawo kwa MMWV	% iliyogawiwa kwa MMWV
2013/14	1,396.8	0	0	0	0	0.0%
2014/15	2,140.9	0	0	0	0	0.0%
2015/16	2,670.2	0	0	0	0	0.0%
2016/17	2,980.9	141.4	141.4	0	282.8	9.5%
2017/18	2,556.8	99.0	133.0	12.0	244.0	9.5%
Jumla	**11,745.7**	**240.4**	**274.4**	**12.0**	**526.8**	**4.5%**

Chanzo: Maendeleo ya Jamii, HWM

Hivi karibuni, serikali imeondoa baadhi ya vyanzo muhimu vya mapato ya Halmashauri kama vile kodi ya majengo, matangazo ya biashara na ushuru wa maegesho ya magari. Hii kwa vyovyote vile itapunguza makusanyo katika Halmashauri nyingi. Ni dhahiri pia kuwa fedha zinazoletwa kwa Halmashauri ni kidogo, hivyo kupelekea Halmashauri kutumia mapato yao ya ndani kulipa gharama za uendeshaji wa shughuli za kila siku za Halmashauri.

Kwa mwaka 2016/17, fedha katika MMWV ziligawanywa kwa usawa kati ya wanawake na vijana, yaani kila kundi lilipata TSH 141.4 milioni. Hata hivyo, Halmashauri iliweka wazi kuwa vijana walipokea ongezeko la jumla TSH 11.5 milioni mwaka 2015/16 na TSH 33.3 milioni mwaka 2016/17 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, na hivyo kupelekea vijana kunufaika zaidi na MMWV kuliko makundi mengine ya walengwa. Mwaka 2017/18 gawio la vijana lilipungua hadi TSH 99 milioni ukilinganisha na wanawake waliopokea TSH 133 milioni huku watu wenye ulemavu wakipata TSH 12 milioni. Hivyo uwiano katika ugawaji wa rasilimali ulizingatiwa kwa kiwango kikubwa. Jumla ya vikundi 49 vya vijana, 98 wanawake na 3 vya watu wenye ulemavu ndio walionufaika na mfuko huo maalum kuanzia mwaka 2016/17.

3.5 Mchango wa MMWV katika maendeleo ya sekta ya kilimo

changanuo unaonesha kuwa 70% ya MMWV ilitumika katika utekelezaji wa shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo kama vile mpunga, ufuta na kilimo cha mbogamboga (10%); ufugaji kuku na wanyama hasa ufugaji wa mbuzi (10%). Matumizi mengine yalikuwa ya usafiri mfano Bajaj na pikipiki (5%), viburudisho na matumizi mengine ya ujasiriamali kama nyenzo za ujenzi zilipokea 5%. Ni wazi kuwa kilimo kimepewa kipaumbele katika mfuko wa mahitaji maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika HWM.

4. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

4.1 Hitimisho

Kumekuwepo na ongezeko la bajeti kwa MMWV kama mwongozo wa serikali ulivyoelekeza, hivyo suala la uwiano wa uwekezaji umezingatiwa. Hata hivyo, ongezeko hili la bajeti halitegemewi kuleta matokeo yanayokusudiwa endapo vikwazo kadhaa havitaondolewa ikiwemo ubadhirifu wa fedha za umma, ukosefu wa elimu ya ujasiriamali, udhaifu katika usimamizi na utunzaji fedha; na ukosefu wa mfumo bora wa usimamizi na tathmini wa MMWV.

Takwimu zinaonesha kuwa bajeti ya kilimo ya HWM siyo ya kutabirika, kitu ambacho kinakwamisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kilimo wilayani. Fedha nyingi zinaonekana katika makaratasi. Hali halisi ni kwamba kuna tofauti kubwa kati ya fedha zilizoidhinishwa na zile zilizopokelewa na HWM, hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa ufanisi wa mipango ya maendeleo ya kilimo wilayani. Kilimo kinachangia kwa sehemu kubwa pato la ndani ya HWM, lakini kwa bahati mbaya sekta hiyo haipokei gawio kutoka HWM kama ilivyostahili.

4.2. Mapendekezo

- Ni wakati sasa wa serikali kuu kusimamia utekelezaji wa mwongozo unaozitaka Halmashauri kuelekeza 20% ya mapato yatokanayo na kilimo kwenda sekta husika, 15% kwenda mifugo na 5% kuelekezwa sekta ya uvuvi. Kwa sasa hakuna hatua madhubuti zinayochukuliwa kwa Halmashauri zisizotekeleza agizo hilo.
- Serikali ibuni aina mbadala ya mikopo isiyo ya kifedha kama vile kukopeshwa matrekta, mashine za kupanda na kuvuna, mbegu bora, vifaa vya kuhifadhi, mashine za ubanguaji, mbolea na pembejeo nyingine zitakazoongeza thamani ya mazao ili kuongeza uzalishaji na tija. Utoaji wa mikopo na misaada mingine kwa wanawake na vijana viambatane na mafunzo ya ujasiriamali.
- Serikali kuu na sekta binafsi waongeze bajeti ya sekta ya kilimo na kutatua changamoto za upatikanaji wa fedha. Aidha serikali kuu inabidi itafakari upya athari zinazotokana na kupungua kwa vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri nchini ikiwemo kudhoofu kwa Halmashauri kifedha.
- Ipo haja ya kuratibu na kutiririsha kazi ya usimamizi na tathmini katika shughuli za idara mbali mbali zinazoshughulika na maendeleo ya wanawake, vijana wa watu wenye ulemavu. Kiasi fulani cha fedha mfano 5% ya fedha za MMWV inaweza kutengwa kwa ajili ya kazi ya usimamizi na tathmini.

Imetafsiriwa na Mbarwa Kivuyo
Imehakikiwa na Magreth Henjewele
©ANSAF & SAIRLA, Septemba 2019

Rejea
Magreth Henjewele (2019) Ripoti ya Uchambuzi wa Bajeti ya Sekta ya Kilimo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Tanzania. Ripoti imeandaliwa kwa ajili ya Jukwaa la Kitaifa wa Kujifunza kuhusu Kilimo Shadidi Endelevu nchini Tanzania, Juni 2019. ANSAF. SAIRLA. Pakua Ripoti kamili kwa kubofya: https://sairla-africa.org/resources/tanzania-nla-mbarali-budget-analysis-study/